# ***Maadui wa wakristo wanaweza kuwashinda sio kwa kushindana mbali, kwa kuafikiana.***

Edmund Burke, mwana filosofia wa Kiingereza ambaye ana umaarufu mwingi alisema, “kitu cha kipekee ambacho kinawezesha uovu kushinda ni wakati watu wazuri hawafanyi jambo lolote.’ Vivyo hivyo, Paulo aliwahimiza waumini kuwa, ‘sisi tu zaidi ya washindi kupitia Kristo atupeaye nguvu., madondoo haya mawili, yanasisitiza kwamba Mungu tayari ametuwezesha kuishi kama washindi katika maisha haya kupitia Yesu Kristo. Ndani ya kila muumini, mnaishi Roho wa Mungu aishiye ambaye anashauku la kutushauri katika kila hatua ya njia yetu. Tishio letu kuu haliko kwa ushambulizi wa shetani, ila kwa kuzembea kwetu kuhusu vipawa na mitaji ambazo Baba Mungu amefanya zipatikane kwa urahisi kwetu

Leo, chukua ushauri wa Paulo kwake Timotheo na uvi chochee upya vipawa vya Mungu maishani mwako, ukijipa moyo kufanya mapenzi Yake. Amsha nafsi na roho yake kuona faida maradufu ambazo Mungu amekupea wewe kupitia kwa Roho Wake na Neno Lake. Mungu anampango mkubwa juu ya maisha yako. Fanya kazi pamoja naye ili ufikie mpango huu wa Mungu.

*Ombi la leo:*

Baba na kushukuru kwa kunitwalia na vyovyote ninavyohitaji ili kupata ushindi kupitia Kristo ulimwenguni. Leo, nachagua kafanya sehemu yangu ili nikupendeze na nikutii Wewe, bila kumpea adui nafasi ya kunishinda mimi. Nisaidie nikuheshimu siku ya leo kwa yote nitakayosema ama kutenda.

*Masomo ya leo*

2 Wakorintho 2:14; Lakini, shukrani kwa Mungu anayetuongoza daima katika msafara wa ushindi wa Kristo

1 Wakorintho 15:57; Lakini tumshukuru Mungu anayetupatia ushindi kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.

2 Wakorintho 2:11; ili tusimpe nafasi Shetani atudanganye; maana twaijua mipango yake ilivyo.

# *Siku zetu za usoni zinategemea yale tunayo yatenda leo*

Maisha yetu ya utangulizi, mahesabu rahisi yalitufunza kwamba, 1+1 = 2 na 2+2=4. Kwa umri mdogo, tuliyakubali haya kwa urahisi na kuyaongeza kwa mwili wetu ulioendelea kukuwa na ufahamu wakimasomo. Maandiko yanatufunza kuwa kila mmoja wetu ni jumuisho la amuzi ambazo tumewahi kufanya maishani mwetu kufikia wakati huu. Tunawakilisha mambo ambayo tumeyawazia, maneno ambayo tumeyasema, na amuzi ambazo tumezifanya. Kwa vile hatuwezi kurudi nyuma na kubadilisha uamuzi wetu wowote, lazima badala yake tuendelee mbele, tukiongezea uchaguzi mpya kuhusu maisha yetu ambao utahusika na maisha yetu milele.

Kama haujapendezwa jinsi ungetaka na jumuisho ya maisha yako leo, fikiria kubadilisha kile unacho ongezea mwenyewe. Mwandishi wa Waebrania anatuchanga moto kwa kusema, ‘ Leo, ukisikia sauti Yake, usifanye moyo wako kuwa mgumu.’ Mungu atakushauri siku ya leo kuhusu kile unafaa kuchagua, akikuelekeza kuhusu mambo ambayo unafaa kukataa na yale unafaa kukubali. Atakushauri kuhusu jinsi unafaa kuelekea. Sikiza mwelekezo Wake kuyahusu maisha yako anapokupa mwelekeo Wake ulio bora zaidi. Kila siku hutupa fursa ya kuanza tena upya.

## *Maombi ya leo:*

Mungu, leo nachagua kukufuata Wewe na kukuheshimu kwa yote ninayo yatenda, ninayo yasema, na yote ninayo wazia. Nisaidie kufanya uamuzi mzuri. Najua siku za usoni wangu zinautegemea.

## *Masomo ya leo;*

Kumbukumbu la Torati 30:19; siku ya leo nimekupea uamuzi kati ya uzima na mauti, kati ya baraka na laana. Sasa naitia mbingu na nchi zishuhudie uamuzi utakaofanya. Chagua uzima, ili wewe na uzao wako muishi.

Zaburi 32:8; nitakushauri na nitakufunza kuhusu jinsi utakavyoenda; nitakushauri na macho Yangu yawe juu yako.

## *Ukomavu ni kuelewa kwamba ingawa itaweza kuhusiana na wewe, sio lazima kila wakati iwe ni juu yako*

Chukua mfano wa mtoto. Wanaimani kuwa mambo yote nikuwahusu. Hulia wakiwa na njaa, usingizi, uchungu, ama wakitaka kubadilishwa mavazi na hawaonyeshi kujali watu wengine kwa chochote. Wanacho kijali sana ni vile watajitosheleza na wawe starehe wakati na saa hiyo. Kwa Wakristo wengi, yaweza kuwa hivyo.

Tunapoendelea kukomaa, twafaa kuanza kutazama maisha na hali zake nyingi kwa mitazamo tofauti. Paulo na Sila walitupwa korokoroni kwa ajili ya kuhubiri injili. Ilikuwa mbaya, inagiza, inaunyevu, inaharufu mbaya, na yakukasirisha. Ingekuwa rahisi kukata tamaa. Ukweli ni kwamba kuwa korokoroni ilimsumbua Paulo lakini akagundua labda haikuwa kumhusu yeye. Wakaamua kumsifu Bwana katika ugumu wao. Mungu akajibu na kuitingiza dunia, akafungua milango ya korokoro, na wengi wakaamini na kuokolewa mpaka yule askari wa jela na jamii yake yote. Wakati mwingine mambo hutusumbua ingawa sio kutuhusu sisi.

### *Ombi la leo:*

Baba nisaidie kukumbana na maisha na mtazamo wa ukomavu. Nisaidie nione umbali zaidi katika barabara ya maisha. Najua wale ambao wanakutumikia watateseka nakusulutishwa na ingawa hiyo inaweza kunifanyikia mimi, sitairuhu iwe nikama yote ni kwa sababu yangu. Naungama kutokuwa na ubinafsi. Mapenzi yako yatendeke wala sio yangu mwenyewe.

### *Masomo ya leo:*

Matendo ya Mitume 16:25,26 ; Karibu na usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakisali na kuimba nyimbo za kumsifu Mungu, huku wafungwa wengine wakiwa wanasikiliza. Ghafla, kulitokea mtetemeko mkuu wa ardhi ambao uliitikisa misingi ya gereza. Mara, milango yote ikafunguka na minyororo iliyowafunga hao wafungwa ikaachana.

2 Wakorintho 8:9; Maana, ninyi mnajua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo: yeye, ingawa alikuwa na kila kitu, alijifanya maskini kwa ajili yenu, ili kutokana na umaskini wake, awatajirishe.

## *Mtazamo wetu maishani unategemea labda ujuzi wetu wa awali ama matarajio yetu ya usoni*

Je, nini kinakufanya uwaze kama unavyowaza kuhusu maisha? Nini kinasababisha uhisi unavyohisi kuhusu jamii yako? Kwanini unataka hicho unachotaka siku ya leo? Je, unafuraha, huzuni, mahangaiko, hofu, huna hisia zozote, ama unashiki kuhusu siku yako? Unahasira, shaka, kero, gandamizo au una ghadhabu ya haraka? Kuna tabasamu kwa uso wako, madaha kwa hatua yako, furaha ndani ya roho yako, na amani ndani ya nyumba yako? Unatarajia siku yako ya leo iwe na mna gani?

Sote husongelea siku yoyote tukiwa na mtazamo na matarajio ya siku hiyo. Mtazamo wetu wamaisha huambatana na ujuzi wetu wa awali ama matarajio yetu ya usoni. Jichunguze mwenyewe na uulize mtazamo wako wa maisha maswali.  Je, kiini chake ni nini? Na, ni mtazamo ambao unampendeza Mungu? Kama sivyo, badilika siku ya leo.

*Ombi la leo:*

Bwana, asante kwa kunipea wakati na kunitia moyo niuchunguze mtazamo wangu na nibadilishe mambo ambayo yanakukasirisha Wewe na kunizuia kupata furaha Yako, amani Yako, na matumaini Yako kuhusu siku yangu. Nifanye niwe kama wewe zaidi.

*Maandiko ya leo:*

Wafilipi 4:8; hatimaye, ndugu zangu, jazeni fikira zenu kwa mambo mema na yanayostahili kusifiwa; mambo ya kweli, bora, haki, safi, ya kupendeza na ya heshima.

Wagalatia 5:22; Lakini matokeo ya kuongozwa na Roho ni mapendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, fadhili, uaminifu,

## *Mitihani tatu ya ufuasi: utiifu, unyenyekevu, uaminifu*

Mungu hatengenezi viongozi…Yeye hutengeneza wafuasi… wafuasi hatengeza viongozi. Ni muhimu tuelewe mitihani mitatu ambayo mfuasi atakumbana nayo katika safari yake yakuhitimu kuweza kuongoza.

Kwanza, mfuasi lazima atii. Kwa kawaida, watu hutii wale wanaotaka ama wale ambao wanao amurishwa kuwatii. Mtihani wapili unahusu kunyenyekea. Unyenyekevu unatulazimu tuweke nguvu zetu na uwezo wetu kwa wale wanaotuongoza hata wakati hatutaki  na kwa uhalisi hatutaki kuwatii. hatimaye, mfuasi lazima awe mwaminifu. Hivi ndivyo ataonyesha kuwa anaunga mkono uamuzi wa kiongozi na ni taji inayo meremeta na  dhibitisho kubwa la tabia ya mtu. Hii inaonekana kutokana na jinsi mtu anavyo ongea na anavyotenda wakati kufuata inagharimu unyenyekevu.

*Ombi la leo:*

Baba, nisaidie niwe mfuasi mkubwa. Nisamehee kwa kutotii huko kwa awali wakati si kuwatii wale wenye mamlaka juu yangu, kutonyenyekea kwangu wakati tulikosa kuelewana na wengine, na mwenendo wangu wakutokuwa mwadilifu  kuliko onekana kutokana na mtazamo wangu na majibu yangu nilipohitajika kunyenyekea.  Ahsante kwa neema na uwezo Wako wa kunisaidia kuwa mfuasi na baraka kwa viongozi walio ndani ya maisha yangu.

*Maandiko ya leo:*

Waebrania 13:7, 17; wakumbukeni viongozi wenu waliowatangazieni ujumbe wa Mungu. Fikirieni juu ya mwenendo wao, mkaige imani yao.

Watiini viongozi wenu na kushika amri zao; wao huchunga roho zenu usiku na mchana, na watatoa ripoti ya utumishi wao mbele ya Mungu. Kama mkiwatii watafanya kazi zao kwa furaha, la sivyo, watazifanya kwa huzuni, na hiyo haitakuwa na faida kwenu.

Wakolosai 3:22; Enyi watumwa, watiini wakuu wenu wa kidunia katika mambo yote, na si tu wakati wanapowatazama kwa kuwa mnataka kujipendekeza kwao; ila fanyeni hivyo kwa moyo wote, kwa sababu ya kumcha Bwana.

## ***Inagharimu ujasiri kuzidi kuendelea***

Bibilia imenakiri hadithi nyingi kuhusu wake kwa waume waliojikuta kwa hali ngumu na zingine za kuaibisha. Tukianzia na Daudi, ambaye watu walitamani kumpiga mawe, tuelekea kwa Esta  alipokabiliana na uwezekano wa kuangamizwa, kila hadithi inatupea sababu zakufanya

tuache kuenda mbele na maisha. Hata hivyo, majemedali wa Biblia na kwa ukweli, majemedali wa imani leo lazima waendelee na safari bila kuangalia hofu zao na makosa yao ya awali.

Inagharimu ujasiri kuendelea na safari  baada ya hali za kuumiza moyo, kuaibisha na kukubalina. Ingawa hivyo, lazima tutafute nguvu za kutuwezesha kuenedelea bila kujalisha hali zilivyo. Jipe moyo rafiki yangu, siku yako kuu, bado iko mbele.

*Ombi la leo:*

Mungu, nahitaji nguvu kuendelea siku ya leo.  Nisaidie kuona zaidi ya wakati huu maishani mwangu na nikuruhusu wewe uponye roho na hisia zangu. Nitumie pia kuwasidia wengine waendelee na wafanyike mashahidi wa uaminifu na upendo Wako.

*Masomo ya leo:*

Zaburi 27:13 ningekuwa nimekata tama, kama singekuwa nimeamini kwamba nitauona uaminifu wa Bwana katika nchi ya walio hai.

Yoshua 1:9; je, sijawaamuru? Iweni wenye nguvu na wenye ushupavu. Msifadhaike; msife moyo, maana Bwana Mungu wako atakuwa na wewe popote uendapo.

## ***Sio unachopitia ila ni jinsi unavyopitia***

Kama kuna kitu kimoja Wakristo wanahitaji, ni ufunuo mpya kuhusu vile tunavyojibu na matendo yetu huhubiri kwa sauti kuliko maneno yetu. Ulimwengu unaotuzunguka una tamani sana kuona nguvu za Mungu. Wanahitaji  kuona imani, ujasiri, nguvu, na upendo ndani yetu tunapokabiliana na uzito wa maisha. Wakati mwelekeo na umakini wetu uko katika shinda zetu za saa hii, jua kwa uhakika mtazamo wa wengine uko kwetu. Hii ni sababu moja kwa nini sio kile tunachopitia ila ni jinsi tunavyokipitia inajalisha.

Kuna mwingine anayeangalia majibu yetu ambaye ni Mungu mwenyewe. Anatamani tuweze kufanana na mfano wa Mwanaye, ambaye kwa sababu ya furaha iliyowekwa mbele Zake, alivumilia msalaba. Tabia yetu wakati tuko ndani ya joto ya vita, inadhihirisha hiyo yake Kristo? Tunabaki imara na watiifu kwa mapenzi ya Mungu na njia zake ama tunakubaliana na mambo tusio yasimamia?  Tazama kile Mungu anaweza fanya ndani yako na kupitia kwako badala ya kuona kile tu kinakutendekea.

*Ombi la leo:*

Baba Mwaminifu, nataka kuwakilisha Kristo kwa wale wanaonizunguka mimi. Nisaidie siku ya leo na kila siku kukumbuka kwamba kile cha muhimu ni vile ninaonyesha ninachoamini kupitia kwa ninachotenda ninapokabiliana na changa moto zile zinazoletwa na maisha.

*Masomo ya leo:*

2 wakorintho 4: 17-18; Taabu tunayopata ni kidogo, tena ya muda tu: lakini itatupatia utukufu upitao matazamio yote, utukufu ambao hauna mwisho. Hivyo tunatazamia kwa makini si vitu vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Maana vinavyoonekana ni vya muda tu; lakini vile visivyoonekana ni vya milele.

Matendo ya Mitume 16:25; Karibu na usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakisali na kuimba nyimbo za kumsifu Mungu, huku wafungwa wengine wakiwa wanasikiliza.

## ***Vyombo ambavyo vimejaa viko katika siku kuu.***

Kanuni moja kuu katika Neno la Mungu ni sheria ya kupanda na kuvuna. Ili tuvune, lazima tupande. Kwa maneno mengine, lazima tumwage tuliyo nayo ili tuzalishe vipawa na tena kuvipa tuzo. Mungu alimpa kila mmoja wetu karama ambazo anatarajia tupeane bure kusaidia kuboresha na kupanua ufalme Wake. Sisi tumejazwa ili tumwagwe ndipo tujazwe tena. Kama hatutajimwaga tubaki watupu, basi labda tunaishi siku yetu kuu.

Usiwe chombo ambacho kimejaa na kinakaa tu na kuokota mavumbi. Kwa uadilifu, jimwage kwa roho ambazo zitakubali na nafsi ambazo zinaumia. Kisha muamini Mungu kukujaza mara nyingine.

*Ombi la leo:*

Mimi ni chombo tayari siku ya leo kumwaga kile ambacho umenipea. Naamini ninapojimwaga, utanifanya upya na kuuisha na unipanue ili ni pokee upako zaidi, kisha nipeane tena. Nitakuwa mwaminifu na kile Utanipea.

*Masomo ya leo;*

Luka Mtakatifu 6:38 ; Wapeni wengine wanavyohitaji, nanyi mtapewa. Naam, mtapokea mikononi mwenu kipimo kilichojaa, kikashindiliwa na

kusukwasukwa hata kumwagika. Kwa maana kipimo kilekile mnachotumia kwa wengine ndicho ambacho Mungu atatumia kwenu."

2 Wafalme 4:3-4; Kisha akasema, 'Enenda uombe vyombo kila pahali, kutoka kwa majirani wako wote- vyombo vitupu; usikusanye vichache. Na utakapoingia ndani,  ufunge mlango nyuma yako na wanao wakiume; kisha uimwage ndani ya vyombo hivyo vyote, na vile vimejaa uweke kado.'

## *Hakuna siku za usoni za kudumu hapa duniani*

Hekima ya Suleimani inadhihirisha utofauti kati ya mtu mwenye hekima na mtu mpumbavu. Anasema mtu mwenye hekima hutazama mbali na kujiadaa mwenyewe kwa sababu ya siku za usoni ilhali mpumbavu ataishi kila siku akitafuta kama kipofu  apate manufaa ya siku hiyo pekee. Kutojipanga kwa sababu ya siku za usoni, Suleimani alisema kutafanya mpumbavu kupata adhabu.

Mfano mkubwa zaidi ni umilele. Utaishi wapi kwa umilele na utapewa kipawa  kiasi gani mbinguni?  Tumia wakati kiasi utafakari maswali haya na ujiandae kwa ajili ya binguni  kwa sababu hakuna siku za usoni za kudumu duniani.

### *Ombi la leo:*

Baba, tafadhali nisaidie  niwekeze kwa vitu vya umilele. Nisaidie kugundua hakuna siku za usoni zaa kudumu hapa duniani. Najua nitavuna kile ninacho panda na kwa hivyo, na weka nathiri kwamba nitapanda mbegu ya umilele ya huruma, wema, amani, na furaha. Baba, nakuamini na ninatazamia zawadi yangu ya umilele.

### *Masomo ya leo:.*

Mathayo Mtakatifu 6:20; Jiwekeeni hazina mbinguni ambako nondo na kutu hawawezi kuiharibu, wala wezi hawaingii wakaiba.

Methali 22:3 ; mwenye busara huyaona mabaya na kujificha;  bali wajinga huendelea mbele wakaumia

## *Unachofikiria chaweza badilisha mawazo yako, unachoamini chaweza badilisha roho yako, lakini ni kile tu unachotenda kinachoweza kubadilisha maisha yako na ulimwengu wako*

Nimesikia kukisemwa kwamba kuna aina mbili za watu; wale wasomi wa historia na wale wanaoitengeneza. Hio ndiyo tofauti ya watu wanaowazia mambo makuu, wanaoamini kuwa ni wakuu,  na wale ambao hutenda mambo makuu. Ukiwazia kuhusu wanadamu ambao wanaumia, labda waweza fanya kitu kuwahusu. Ukiamini kuwa una hekima na uwezo wa kunenea  hitaji hiyo labda utapata msukumo Fulani. Hata hivyo, kama hautafanya jambo maalumu kuhusu shida hii; ulishe mtu mwenye njaa, uwape maji wenye kiu, uhubiri injili kwa wale masikini, uwaponye wagojwa, ama uwaweke mateka huru, haujafanya chochote kusaidia.

Pata ashiki na kisha uwe na mpango, lakini isiishie pale.  Weka miguu kwa imani yako na uhusike kwa kazi ambayo ni mikono yako pekee inaweza kufanya.

### *Ombi la leo*

Baba, nipe ashiki yako Kwa sababu ya dunia ambayo imepotea na inaumia, nionyeshe mpango wako na jinsi ninavyoweza kuhusika, na kisha, Bwana, niweke katika shamba lako la mavuno kama mfanyi kazi. Nataka nikufanyie kazi Wewe.

### *Masomo ya leo;*

Waraka wa Yakobo 1: 22-27; Msijidanganye wenyewe kwa kusikiliza tu neno lake, bali litekelezeni kwa vitendo Yeyote anayesikiliza hilo neno lakini halitekelezi, huyo ni kama mtu anayejiangalia sura yake mwenyewe katika kioo. Hujiangalia mwenyewe, kisha huenda zake, na mara husahau jinsi alivyo.Lakini mtu anayeangalia kwa makini sheria kamilifu ambayo huwapa watu uhuru, mtu anayeendelea kuizingatia, na si kuisikia tu na kuisahau baadaye, bali anaitekeleza, mtu huyo atabarikiwa katika kila kitu anachofanya.Kama mtu akijiona kuwa ni mtu mwenye dini, lakini hawezi kuutawala ulimi wake, dini yake haifai kitu, na anajidanganya mwenyewe. Dini iliyo safi na isiyo na hitilafu mbele ya Mungu Baba ni hii: Kuwasaidia yatima na wajane katika shida zao, na kujilinda mwenyewe usichafuliwe na ulimwengu huu.

## *Maisha ni ubashiri*

Maisha ni safari na kama safari nyingine yoyote, barabara tunayoipitia haifai kuchaguliwa kwa bahati na sibu ama kwa kupita kiwango. Kwa vile kila barabara hutuelekeza pahali ambapo panaweza bashirika, ni muhimu kuchunguza njia ya maisha yetu ili tusije tuka shtuka wakati tunafika mwisho wa safari yetu. Mtu ambaye anafuata njia ya uwongo, undanganyifu, wizi, ama ya kukubaliana asichanganyikiwe akijikuta bila rafiki, kazi ama akiwa jela…. Hapo ndipo barabara hiyo huishia.

Katika hali hiyo, wakati wowote maishani, mtu aweza badilisha barabara aipitiayo na kugeuza maisha yake. Wacha Neno la Mungu liangazie njia za maisha yako leo na uishi na matumaini ukielekea hatima yako.

*Ombi la leo:*

Mungu, ninakushukuru kwa kuwa pamoja na mimi katika safari yangu bila kujalisha njia niliyoifuata. Hata hivyo, naomba unipendue kutoka kwa njia yangu mwenyewe na unielekeze kwa njia Yako kuhusu maisha yangu. Nionyeshe mapenzi Yako kwangu.

*Masomo ya leo;*

Zaburi 119:105; Neno Lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu.

Mithali 14:12; iko njia ionekanayo kuwa bora machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti.

Zaburi 27:11; Ee BWANA, unifundishe njia yako, Na kuniongoza katika njia iliyonyoka, kwa sababu ya wanaoniotea.

# ***Maisha Ni uamuzi***

Katika kuamini-uamuzi wa Imani ulio katika misingi ya Ushauri wa uuguzi, jambo la kwanza Ni kuhakikisha kuwa tuna amini kile Neno la Mungu linasema na sio kile maadui wa Mungu wanasema kutuhusu sisi na hali zetu maishani. Aidha inaongea kuhusu kuthibiti hasira, tabia za uzoefu, ama mienendo ya uasi na matendo, tunachoamini kitathibitisha jinsi tunavyowaza, tunavyohisi, na tunavyotaka.

Hata hivyo, maisha ni uamuzi, na ingawa tuna amini ukweli wa Neno la Mungu, lazima bado tuamue kufanya Neno Lake. Imani bila kufuatwa na matendo ni bure na kuamini pasipo kuamua kutii Neno la Mungu haimanishi chochote.

*Ombi la leo;*

Mpenzi Bwana, nisaidie nijue Neno Lako, niamini Neno Lako na kisha nichague kufanya mapenzi Yako. Sitatoa visababu tena vya kutofuata sheria Zako. Ahsante kwa msamaha wako.

*Masomo ya leo*

Waraka wa Yakobo 2:18; Lakini mtu anaweza kusema: "Wewe unayo imani, mimi ninayo matendo!" Haya! Nionyeshe jinsi mtu anavyoweza kuwa na imani bila matendo, nami nitakuonyesha imani yangu kwa matendo yangu. Je, wewe unaamini kwamba yuko Mungu mmoja? Sawa! Lakini hata pepo huamini hilo, na hutetemeka kwa hofu. Mpumbavu wee! Je, wataka kuonyeshwa kwamba imani bila matendo imekufa?

## ***Huenda ukahitaji mapumziko, kabla haujavunjika ukielekea kwa upenyo wako.***

Wakati mwingine jambo la uungu unachohitaji kufanya ni kupumzika. Hebu wazia wewe ni mwana riadha mwenye umaarufu duniani na unaelekea mbio yenye umuhimu sana kwa maisha yako. Jambo hili litachukua nguvu zako zote za mwili, mawazo, nguvu za hisia zako na mtazamo wote ulio nao. Usipopata wakati unao tosha mapumziko, unafikiria utendaji wako utakua kiwango gani?

Mbaribari ( mwinuaji uzito mwenye umaarufu duniani) alikua akisema, ‘ hakuna kitu kinaitwa mafunzo yaliyo zidi, ni kukosa usingizi tu, kutokula chakula kizuri, na kutokuwa na mori.’ Wakristo wengi leo wanakula vizuri Neno la Mungu na wana mapenzi ya kutenda kazi ya Mungu, ila maisha haya yanawamaliza polepole. Labda tunahitaji kupunguza mwendo na kuwa na wakati wa mapumziko maishani. Ufanisi ni wakati fursa inakutana na uandalizi. Jiandae hata wakati inamaanisha uwe na wakati wa mapumziko.

*Ombi la leo;*

Baba, naomba unisaidie kupata wakati wa mapumziko. Najua utanihitaji siku za usoni na ninataka niwe tayari. Nisaidie niwe na mkakati ambao utanihifadhi kwenye mchezo miaka mingi ijayo. Nataka nilete utofauti wahali ya juu ninaoweza kuleta kwa ufalme wako, jamii yangu, na siku zangu za usoni.

*Masomo ya leo;*

Kutoka 23:12 ; siku sita utafanya kazi yako, na siku ya saba utapumzika; ili kwamba ng'ombe wako na punda wako wapate kupumzika na, kisha mwana wa mjakazi wako na mgeni wapate kuburudika.

Mathayo Mtakatifu11:28-29; Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jifungeni nira yangu, mkajifunze kwangu, maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtatulizwa rohoni mwenu.

## ***Mungu huita ukuu kutokana na uduni***

Kama yule kijana mdogo mchungaji wa ng'ombe aliyeitwa Daudi aliyekuwa pekee akiwaangalia kondoo wachache huko nyuma jangwani na yule hatimaye alifanyika kuwa mfalme wa Israeli, Mungu ana watayarisha watu walio duni. Inaonekana Mungu anapenda kuwashangaza watu na maarifa yanayofanyishwa kazi.

Saa hivi Mungu ana watayarisha wale Atawatumia siku moja, labda wewe ndiye anataka kutumia. Jipeane kwa uandalizi wake, fanyika mkuu katika maisha yako ya ukawaida wa kila siku na usipuuze siku za mwanzo mdogo. Mungu ana shughuli ya kuunda ufalme Wake na wafalme Wake wa siku zijazo.

*Ombi la leo;*

Mungu, najua kila wakati una uangalifu unaponiwazia na jinsi ninavyo weza kutumikia Ufalme Wako vizuri. Niandae, ewe Bwana, ili niwe tayari siku ya vita. Nipe hekima nisiweze kugandamizwa bali niweze kuelimishwa na kutiwa motisha kwa siku kuu za maisha yangu.

*Masomo ya leo;*

Isaya 49:2; Naye anifanya kinywa changu kuwa kama upanga mkali; katika kivuli cha mkono wake amenisitiri; naye amenifanya kuwa kama mshale uliosuguliwa; katika podo lake, amenificha.

Wafilipi 1:6; nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi jema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu.

Zaburi 138:8; BWANA atanitmiliza mambo yangu; Ee BWANA fadhili zako ni za milele; usiziache kazi za mikono yako.

## *Yakiachwa yenyewe, mambo mabaya hayafanyiki mema ila huharibika zaidi*

Kama gari linalohitaji kurekebishwa ama boma linalohitaji kusafishwa, maisha yetu hayawi mema, masafi, ama yenye faida zaidi peke yake… inagharimu kazi. Kuyaweka kado hadi wakati unaopendeza zaidi, haifaidi chochote. Hayata jitengeneza yenyewe.

Yakiachwa yenyewe, mambo mabaya hayafanyiki mema, ila huharibika zaidi. Hii ndiyo sababu lazima taungalie kwa umakini mambo yale yanahitaji kazi na tutie jitihada za kuya tengeneza. Kama ni mtazamo, matendo, mawazo, ama hisia, twafaa tujichunguze kisha tujilazimishe kuleta mabadiliko tunayojua ni ya umuhimu. Anza utaratibu huu leo.

*Ombi la leo;*

Baba, Neno Lako husema kwamba leo ndio siku ya wokovu na sasa ndio wakati unaokubalika. Nionyeshe mambo yale yanahitaji umakini wangu katika maisha yangu na unipe neema na uwezo kufanya kitu kuhusu mambo haya siku ya leo. Nielekeze, hatua baada ya nyingine, siku baada ya nyingine, nifanyike wakupendeza zaidi na mwenye manufaa mikononi Mwako.

*Masomo ya leo;*

1 Wakorintho 9; 24-27; Je, hamjui kwamba katika uwanja wa michezo, ingawa wapiga mbio wote hukimbia, ni mmoja tu anayejinyakulia zawadi? Wanariadha hujipa mazoezi na nidhamu kali; hufanya hivyo ili wajipatie taji iharibikayo! Lakini sisi twafanya hivyo tupate taji ya kudumu daima Ndivyo basi, ninavyopiga mbio nikiwa na nia ya kushinda; ndivyo ninavyopigana, na si kama bondia anayetupa ngumi zake hewani.Naupa mwili wangu mazoezi magumu na kuutia katika nidhamu kamili, nisije mimi mwenyewe nikakataliwa baada ya kuwahubiria wengine.

## *Upendo ni kazi… na lazima tufanye kazi yetu ya kwanza ili tuupate upendo wetu wa kwanza*

Inasemakana sana kuwa, ‘ ulichofanya kukuwezesha kukipata, ndicho unahitaji kufanya ili ukihifadhi.’ Naamini huu ni ukweli. Kutoka kwa ndoa, hadi kwa bishara, kinacho gharimika ili kipatikane, ndicho kinahitajika ili kukitunza.

Upendo ni kazi… na ni lazima tufanye kazi yetu ya kwanza ili tuupate upendo wetu wa kwanza. Hii inahusu vile tunatazama wokovu wetu, kanisa letu, jamii yetu, na Mungu wetu. Wakati mambo yana onekana kama sio mazuri sana ama kana kwamba kuna kitu ambacho hakiko-jiangalie mwenyewe: umekuwa ukitumia muda unaohitajika kuwekezewa maeneo haya kama ulivyofanya hapo awali? Kama sivyo, ndio sababu kuna kitu kina kosa. Rudi tena kwa msingi na uanze kufurahia maisha tena.

*Ombi la leo:*

Bwana, nionyeshe sehemu za maisha yangu ninakohitajika kutumia wakati maalum. Nihuisha na unipe ufufio, ewe Mungu. Fanya upendo wangu kama chemichemi inayo bubujika maji kila wakati ambayo inaleta raha na kuhuisha nafsi yangu na za wale nikutanao nao. Nihuishe, ewe Bwana.

*Masomo ya leo:*

Matendo ya Mitume 3:19; Basi, tubuni mkamrudie Mungu ili afute dhambi zenu. Fanyeni hivyo ili Bwana awape nyakati za kuburudika rohoni na kuwaletea yule Kristo aliyemteua ambaye ndiye Yesu.

Isaya 57:15; maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye jina Lake ni mtakatifu; asema hivi, 'nakaa Mimi pahali palipoinuka pahali patakatifu; tena pamoja nay eye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo ya walio tubu.

## *Ukristo ni imani inayogharimu matendo.*

Siku moja niliambiwa ya kwamba neno "kuamini" ni kinyume na neno kutokuamini. Kutokuamini kuna maanisha, kutokutimiza madai. Nilielezwa ya kwamba neno "kuamini" limetengenezwa na maneno mawili yanayojulikana kama: ku na amini. Huo ndio msingi wa maana wa neno ambalo mwamini atakua ni mtu ambaye ameishi kile alicho… mu-umini.

Kama hii ni kweli, Mkristo muumini atakuwa ni mtu ambaye ameshikamana sio tu na imani lakini pia kwa matendo ya Kristo. Ukristo, ni imani ambayo inagharimu matendo. Unatenda kama mkristo?

*Ombi la leo*

Mungu, najua unanipenda na upendo wako kwangu haujawekwa kwa misingi ya matendo lakini kwa neema. Hata hivyo, nataka kukufurahisha na chochote ninachofanya. Naomba Bwana kwa upole uniongeze kuona pale sioni kama Mkristo na unisaidie kuwachilia mawazo yangu na matendo yangu na kuyaleta katika kukubaliana na mapenzi Yako.

*Maandiko ya leo:*

2 Petro 2: 2; Tena watu wengi watazifuata hizo njia zao mbaya, kwa sababu yao, wengine wataipuuza Njia ya ukweli.

2 Wakorintho 10:5; na kubomoa kila kizuizi cha majivuno kilichowekwa kuipinga elimu ya Mungu; tunaziteka fikira zote na kuzifanya zimtii Kristo.

Wakolosai 3:17; Na, kila mfanyacho kwa neno au tendo, fanyeni vyote kwa jina la Bwana Yesu na kumshukuru Mungu Baba kwa njia yake

## ***Ni Mungu pekee awezaye kupima kazi iliyomalizika.***

Usiwe mgumu kwako mwenyewe. Kama ni mbaya, ni hakika Mungu bado hajamaliza. Wazia vile ingeonekana kama kitu kinaweza simamishwa kama bado hakija maliza utaratibu wa uundaji na kikachanganywa na vile vimekamilisha uundaji. Bila shaka kutaonekana makosa ya uwazi. Ni muumbaji pekee anaye fahamu uumbaji unapokamilika.

Ni Mungu pekee anayeweza kupima kitu ambacho kimekamilika. Usiogope, Mungu hajamaliza na wewe bado na anakupenda sana kiasi cha kuwa hawezi akakuwacha vile ulivyo wakati huu. Bado anakutendea kazi!

*Ombi la leo:*

Nifunze, Ewe Mungu, kuto ghadhabishwa na utaratibu wa maisha. Najua unafanya kazi nami kwa hekima na umaarifa ili nitamani na niweze kufanya mapenzi Yako. Naamini kwamba utafanya mambo yote yapendeze kwa wakati unao faa. Ndio haya maisha yangu, Bwana… fanya kitu kutokana nayo kama Utataka.

*Masomo ya Leo;*

Isaya 64:8 ; lakini sas, Ee BWANA, wewe u baba yetu; sisi tu undongo, nawe u mfinyanzi wetu; sisi sote tu kazi ya mikono Yako.

Yeremia 18:4; na chombo kile, alochokuwa akikifinyanga, kilipoharibika mkononi mwake yule mfinyanzi, alikifanyiza tena kuwa chombo kingine, kama alivyo ona vema yule mfinyanzi kukifanya.

Zaburi 138:8; Bwana atanitimizia mambo yangu; Ee BWANA, fadhili zako ni za milele; usiziache kazi za mikono yako.

Wafilipi 1:6; basin ina hakika kwamba Mungu aliyeanza kazi hii njema ndani yenu ataiendeleza mpaka ikamilike katika siku ile ya Kristo Yesu.

## *Leo huenda ni fursa yako ya kuwajua baadhi ya watu wakubwa zaidi ambao haujawahi kuwaona*

Kila siku, sisi huwapita watu njiani, sokoni, shuleni, ama kazini… watu hatujawahi kutana nao ama hatujawahi pata nafasi ya kuwajua. Baadhi ya watu hawa wana uwezekano wakufanyika marafiki wa karibu ambao mtu anaweza kuwa nao. Kila mmoja wao ana hadithi, tumani, ndoto, masumbuko, na mapenzi anayoweza kutaka kushiriki na wengine.

Huenda leo ni fursa yako ya kuwajua baadhi ya watu wakubwa zaidi ambao haujawahi kuwaona. Kwa nini usichukue nafasi hii na uwekezee kwa kuwafanya marafiki wengine wapya. Mara nyingi, watu hupenda kuongea mambo yao wenyewe na, kama unajali, watashiriki. Chukua jukumu, kuwa makini, sikiza na uonyeshe kuelewa kunako maanisha.siku zijazo, utafurahia.

*Ombi la leo:*

Bwana Mungu, naomba kwamba uniwezeshe kutengeneza husiano njema na za kiungu ambazo zitadumu maisha yote. Nihuishe leo na uniongoze kwa watu wafaao. Nipe wale naweza badilisha na wale wanao weza kunibadilisha kwa uungu.

*Masomo ya leo:*

Muhubiri 4:9; afadhali kuwa wawili kuliko mmoja; maana wapata ijara njema kwa kazi yao.

Mithali 17:17; rafiki hupenda siku zote.

Mithali 18:24; ajifanyiaye rafiki wengi ni kwa uangamivu wake mwenyewe; lakini yuko rafiki aambatanaye na mtu kuliko ndugu.

## ***Labda tunatoka kwa siku kuu yetu, ama tuko kwa siku kuu yetu, au twaelekea siku yetu kuu... na ukweli ni kwamba, ni uamuuzi wetu***

Mambo mengi maishani ni kuhusu mtazamo. Inaonekana kuwa nusu ya kwanza ya maisha ya mtu hutumika akitafuta fanaka na nusu ya pili hutumika akitafuta umaana. Ingawa kila siku tunapata njaa ya kufikia kiwango fulani cha ufanisi na utabulikanaji, twaweza kubaki watupu, hata tukiwa na mafanikio hayo.

Siwezi kutaka kutumia maisha yangu yote nikipanda ngazi kisha nikifika kilele nigundue kumbe iliegemea jengo lisilofaa. Mungu ana mpango ambao unakuhusisha wewe. Anatenda kazi ndani ya kila mmoja wetu sasa hivi kufanya kitu kikubwa zaidi kuliko kile tumewahi ona umbali huu. Kuwa na ujasiri kuwa siku njema bado iko mbele yako. Ukweli ni kwamba, tukipumua pumzi yetu ya mwisho duniani, tunaweza kukiri na ushupavu kuwa siku yetu kuu bado iko mbele. Ni uamuzi!

### *<u>Ombi la leo:</u>*

Baba, mimi sijakamilisha bado. Nataka niwe mkuu katika ufalme Wako na maisha yangu yaweze kuhesabika. Nipe maono na ndoto zaidi ya hali nilizo nazo sasa hivi. Nipeleke kwa siku yangu kuu.

### *<u>Masomo ya leo:</u>*

Yoeli 2:28 ; hata itakuwa baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono. Tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake katika siku zile; nitamimina roho yangu.

Yeremia 29:11; maana ninajua mawazo ninayo wawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.

## ***Wakati kandarasi inalinda wema wangu kwa gharama ya wengine, agano huahidi uzuri wa wengine kwa gharama yangu***

Watu wengi hungia katika husiano na mawazo ya kandarasi. Kandarasi za eleweka kuwa muhimu katika husiano nyingi za kibiashara. Hata hivyo, kandarasi haina sehemu katika uhusiano wa kibinafsi. Chukua mfano wa ndoa, maandikiano yamekuwa ni kama mtindo wa jamii za siku hizi. Kusikizana huku kwa kuandikiana, hakuna tofauti na kandarasi inayotengenezwa ili kulinda upande huu kutokana na ule mwingine. Sheria, haki, na majukumu huwa zinatamkwa na ghadhabu kwa yule asiyezifuata.

Mungu aliunda ndoa na husiano zingine za maana, zizaliwe na kutunzwa kwa njia ya maagano. Agano sio uhusiano wa 50/50…. Mbali ni 100/100. Kila mtu ana jukumu la kutenda nafasi yake ya 100% bila kujalisha mwenzake katika uhusiano huu anafanya aje. Agano ndilo Mungu alimpa Iburahimu na ndilo Yesu anatupa siku ya leo. Heshimu uhusiano wako wakiagano… Mungu huheshimu.

*<u>Ombi la leo:</u>*

Baba, nataka niwe mhusika wa agano na Wewe kwa kufanya husiano za kiroho ambazo zitadumu milele. Nifunze kuhusu agano na uniwekee watu wafaao katika maisha yangu. Nipe neema ya kudhamini husiano zangu zaidi ya jinsi zinavyoweza kuninufaisha mimi.

*<u>Masomo ya leo:</u>*

Wafilipi 2:4 kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo yaw engine.

1 Samweli 18:1; ikawa Daudi alipokwisha kusema na Sauli, roho ya Yonathani, ikaambatana na roho ya Daudi, Yonathani akampenda kama roho yake mwenyewe.

## ***Wakati Mwingine Mungu anatutarajia tupate ushindi katika hali kabla tupate tushinde hali zetu.***

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwa, mradi walikuwa duniani hii, lazima wangekutana na mateso, lakini wawe na furaha kwa sababu aliushinda ulimwengu. Kushinda ukiwa ndani ya mateso, majaribu, na mitihani ni utaratibu wa hatua mbili. Kwanza, kuna ushindi tunaoweza kupata hata kabla hatuja kobolewa na husukumwa na hali zetu. Ushindi huu hautokani na kubadilika kwa hali zetu ila sisi kubadilika tukiwa ndani ya hali zile. Ushindi huu huimarisha imani yetu. Ushindi ndani ya hali zetu ni kama utangulizi tu wa kupata ushindi na kuona hali zikibadilika kutupea kibali.

Wakati mwingine Mungu anatu tarajia tupate ushindi ndani ya hali kabla tushinde hali zetu. Pata mtazamo wa kimawazo kamili kuhusu kuwa na Mungu kwa upande wako. Kwa kuwa, Mungu akiwa upande wako, nani aweza kufaulu kuwa kinyume na wewe?

*Ombi la leo:*

Mungu, najua kuwa hautaniacha na wala kunitupilia mbali. Maisha yangu, furaha yangu, usoni mwangu, na kufanikiwa kwangu hakugharimu hali za maisha yangu. Naamini kuwa nikiwa na Wewe mambo yote ya wezekana. Nineemeshe kuona kazi Yako iliyokamilika ndani yangu, hata kabla nione mambo yakibadilika.

*Masomo ya leo:*

Yohana 16:33; Nimewaambieni mambo haya ili mpate kuwa na amani katika kuungana nami. Ulimwenguni mtapata masumbuko; lakini jipeni moyo! Mimi nimeushinda ulimwengu!"

Zaburi 34:19; mateso ya mwenye haki ni mengi,lakini BWANA humponya nayo yote

Warumi 8:31b Mungu akiwa upande wetu, ni nani atakuwa kinyume na sisi?

## ***Wenye maono huishi siku za usoni***

Usiache maisha yawekee maono yako kiwango cha chini. Katika Zaburi 78 mstari wa 41 Daudi ana nena kuhusu wana wa Israeli wakiwekea Mung kiwango na uwezo Wake kuwasaidia. Inasema kuwa walimjaribu Mungu, na wakamgeukia na kuwekea kiwango Mtakatifu wa Israeli. Mwanadamu aweza je kuwekea Mungu kiwango? Kwa kuweka maono yetu juu ya kile tunaona badala ya kile Mungu anacho ona.

Twafaa kukumbatia ukweli wa Mungu kama ukweli wetu. Hii huwezekana wakati tunakumbatia maono Mungu aliyo nayo kwetu badala ya kuruhusu hali zetu za sasa kutoweza kwa maisha kutuamurishe. Uliza Mungu akuhuishe zaidi ya wakati huu na maono Yake kuhusu siku za usoni wako na utoe viwango kwa Mungu.

*Ombi la leo:*

Mungu, naomba unihuishe na maono Yako kuhusu siku zangu za usoni. Nionyeshe maisha yangu kama unavyo yaona Wewe na ukunjue ndoto Yako kupitia kwangu. Naamua kutoa viwango na kukufanya uwe kielelezo changu.

*Masomo ya leo:*

Ayubu 33:14-15; kwa kuwa Mungu hunena mara moja, naam hata mara ya pili ajapokuwa mtu hajali. Katika ndoto, katika maono ya usiku, usingizi mzito uwajiliapo watu katika usingizi kitandani.

Habakuku 2:2; kisha MUNGU akanijibu na kusema, 'iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji

## *Na Ufalme wako uje*

Ufalme wa Mungu hauji kwa mtazamo, sio pahali panapogusika, lakini uko ndani yako. Ufalme huu huzaa haki, amani,na furaha na hupatikana popote alipo Yesu. Ni wajibu wetu kuleta maisha yetu chini ya mamlaka makuu ya Mungu kwa kuwa kokote anakotawala, pale ufalme wa Mungu hupatikana.

Maandiko yanatuambia tusisumbuke zaidi ya inavyopaswa kuhusu kile tutakachokula, tutakachokunywa, ama mavazi tuyavaayo. Tunafaa kutafuta kwa nafasi ya kwanza , ufalme wa Mungu na kusimama na Yeye sawasawa na haya mengine tunayoyahitaji yataongezewa katika maisha yetu kutokana na utele Wake. Fuata mfano wa Yesu unapo omba na useme, 'Ufalme Wako uje na Mapenzi Yako yatendeke.'

*Ombi na somo la leo:*

Mathayo 6:9-13;  Basi, hivi ndivyo mnavyopaswa kusali: `Baba yetu uliye mbinguni: Jina lako litukuzwe.Ufalme wako ufike. Utakalo lifanyike duniani kama mbinguni.Utupe leo chakula chetu tunachohitaji.Utusamehe makosa yetu, kama nasi tunavyowasamehe

waliotukosea.Usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule Mwovu. Kwa kuwa ukiwasamehea wanadamu wanapokukosea, Baba wako wa mbinguni atakusamehea hata wewe. Lakini kama hauta wasemehea wanadamu wakikukosea, Baba yako hatakusamehea.

## *Usipuuze mwanzo mdogo*

Mungu ameitengeneza ili kila mbegu iwe na uwezo wa kujijumuisha, na kupeana mbegu kwa vizazi vijavyo. Kama ikipewa fursa, iwekwe kwa ondongo wenye rotuba, kwa wakati unao faa, inyunyuziwe maji na kupaliliwa vizuri, mbegu hii ina iwezo wa kutimiza hatima na kuwa zaidi ya ilivyoonekana kwanza.

Jiruhusu pia fursa kama hiyo. Kuna mengi zaidi kwa mwito wako, usoni mwako, na utendaji wako kuliko yale unafahamu. Mpe Mungu shukurani kiasi. Anampango na amekuchagua Wewe kama mbegu Yake kwa ajili ya usoni mkuu.

*Ombi la leo;*

Mpenzi Mungu, sina uwezo wa kuuona mwisho kutokana na mwanzo kama jinsi unavyo ona.  Hata hivyo, nionyeshe njia Zako na unipe neema Yako nipande maisha yangu kama mbegu kwa kazi ya kizazi hiki  ili iwe mavuno kwa vizazi vijavyo. Sitapuuza siku za mwanzo mdogo.

*Masomo ya leo:*

Luka Mtakatifu 13: 18-19;. Yesu akauliza: "Ufalme wa Mungu unafanana na nini? Nitaulinganisha na nini? NI kama mbegu ya haradali aliyotwaa mtu mmoja na kuipanda shambani mwake; ikaota hata ikawa mti. Ndege wa angani wakajenga viota vyao katika matawi yake."

Isaya 46:10; nitangazaye mwisho tangu mwanzo, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado, nikisema, shauri langu litasimama, nami nitatenda mapenzi yangu yote.

## *Hautafanya vyema kuliko mapenzi ya Mungu Kwako*

Wakati watu wengine wanatafuta kufaulu katika maeneo Fulani ya maisha, iwe ni kielimu, ki uchumi, kikawaida, ama kwa mambo mengine ya kibinafsi, tayari Mungu ameweka ukuu na fanaka ndani ya kila mtoto

Wake. Kinacho faulu kwa mtu mmoja chaweza kosa kufaulu kwa mwingine na 'kuwa tajiri haraka' ni mtindo unao elekeza wengi wenye kuufuata kwa shida. Wakati huu wote, barabara ya kipekee inayo tuelekeza kwa fanaka ya kikamilifu na kutosheleka  na kutafuta na kufuata makusudio ya Mungu kwa maisha yako.

Wacha kufuata fanaka kwa kuenda njia yako mwenyewe. Huwezi kupata hekima kuliko Mungu ama uwe na furaha kuliko kuwa tu ndani ya mapenzi Yake.

*Ombi la leo:*

Nionyeshe njia Yako Mungu Baba na unidhihirishie mapito Yako kuhusu maisha yangu. Wacha maisha yangu yasiwe kama matokeo ya ufahamu duni tu wa mwanadamu ama mzunguko mbali uwe njozi inayo kunjuka ambayo Wewe pekee ndiwe waweza kuandika na mimi naweza kufuata.

*Masomo ya leo:*

Mithali 3:5-7; mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe. Katika njia zako zote, mkiri Yeye, naye atayanyosha mapito yako. Usiwe mwenye hekima machoni pako, Mche BWANA, ukajiepushe na uovu.

Yakobo 4:13-15; Basi, sasa sikilizeni ninyi mnaosema: "Leo au kesho tutakwenda katika mji fulani na kukaa huko mwaka mzima tukifanya biashara na kupata faida." Ninyi hamjui hata maisha yenu yatakavyokuwa kesho! Ninyi ni kama ukungu unaotokea kwa muda mfupi tu na kutoweka tena. Mngalipaswa kusema: "Bwana akitujalia tutaishi na tutafanya hiki au kile."

## ***Ukuzi na upanuzi husimama wakati wale wenye huduma hawawezi ama hawataki kuzaa***

Katika kitabu cha matendo ya mitume, ni maelezo kuhusu mwanzo wa kanisa. Ilikuja kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Uzazi wa kanisa ni jukumu Mungu alijipea Mwenyewe ilhali kukua na kupanuka kwake kuliachiwa kimsingi wale walioitwa na Mungu, akawahami, na kuwatuma.

Lazima tukae tukijua upanuzi wa kanisa unaletwa na kanuni yetu kuwa tumebadilishwa na Nguvu zake na kujumuisha mabadiliko haya ndani

ya wengine kupitia ushuhuda wetu na matendo yetu. Huduma ni yako wewe.

*Ombi la leo:*

Bwana Yesu, nitatembea kwa nguvu za Roho Wako Mtakatifu. Naachilia kazi za mikono yangu na mipango ya maisha yangu kwa makusudio Yako ya kiungu. Nakualika uingiliae kati kwa hali zote za maisha yangu ambako ufahamu wangu na mtazamo wangu ni wakiwango cha chini. Nisaidie nizalishe ndani ya watu wengine kile umezalisha ndani yangu.

*Masomo ya leo:*

Matendo ya Mitume 1:8; Lakini wakati Roho Mtakatifu atakapowashukieni ninyi, mtajazwa nguvu na mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, katika nchi yote ya Yudea na Samaria, na hata miisho ya dunia."

1 Petro 4:10; Kila mmoja anapaswa kutumia kipaji alichojaliwa na Mungu kwa faida ya wengine, kama vile uwakili mwema wa zawadi mbalimbali za Mungu.

Mathayo Mtakatifu 28:19-20; Nendeni basi, mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wanafunzi wangu; mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.Wafundisheni kushika maagizo yote niliyowapeni. Nami nipo pamoja nanyi siku zote; naam, mpaka mwisho wa nyakati."

## ***Fanaka ni zaidi ya utaratibu wa hatua moja***

Wakati Mungu alitaka kuumba ulimwengu Wake mkamilifu, hatua Yake ilianza wakati alisema, ‘ na iwe nuru.’ Zaidi ya siku saba za uumbaji zilizo fuata, aliendelea akichukua hatua baada ya nyingine hadi alipo pata matokeo aliyokuwa ameyatamani. Maishani mwetu mwote, sisi pia tunachangwa moto tufikie malengo yetu kwa kutengeneza na kukumbatia hatua zinazohitajika ili tufanikiwe. Iwe ni kwa kujenga nyumba, kuchukua safari, ama kulea jamii, jukumu lenye fanaka hukamilika hatua baada ya hatua yenye kubatilika.

Fanaka ni zaidi ya utaratibu wa hatua moja na mara nyingi fanaka ni ya wale ambao wamekubali kukumbatia na kuvumilia utaratibu huo. Ni hatua gani itagharimu ili maisha yako yaweze kufaulu?

*Ombi la leo;*

Bwana, nisaidie kutoshushwa moyo ndani ya utaratibu wa maisha. Nionyeshe njia zako na unipe hatua naweza kuchukua ili nifaulu mbele ya macho Yako. Nisaidie kuwa na subira na unipe neema ya kuvumilia safari.

*Masomo ya leo:*

Zaburi 37:23-24; hatua za mtu za imarishwa na BWANA, naye aipenda njia yake, ajapojikwaa hataanguka chini, BWANA humshika mkon na kumtegemeza.

Zaburi 37:31; Sheria ya Mungu wake imo moyoni mwake, hatua zake hazitelezi

2 Samueli 22:37; umezifanyizia nafasi hatua zangu, wala miguu yangu haikuteleza.

## *Mungu hutembea kupitia watu hadi wengine*

Katika sura ya tisa ya Matendo ya Mitume, Saulo wa Tarsusi alikuwa akielekea Damasiki kuendelea kuwahangaisha Wakristo. Nuru kuu ikampofisha na akasikia sauti toka mbinguni. Sauti hii Akajitambulisha kama Yesu na akaamurisha Saulo kuenda mjini na angonjee maagizo kupitia mtu mwingine, ambaye baadaye alitambulika kama Anania. Katika Matendo ya Mitume sura ya kumi, mtu aliyeitwa Korinelio alitembelewa na malaika na kuagizwa amtumaniye mtu aitwaye Petro, ambaye angemweleza jinsi ya kuokoka.

Katika hadithi hizi na zingine, sio sauti ya mbinguni iliyowafundisha watu hawa njia ya Kristo, ila fursa hii na jukumu ya kushuhudia na kufanya wanafunzi ilipewa watu wengine. Unaona, Mungu hutumia watu kuwafikia wengine. Ruhusu Mungu afikie mtu mwingine kupita kwako siku ya leo.

*Ombi la leo;*

Mpenzi Bwana, ahsante kwa kunipea fursa ya kuwaambia wengine kukuhusu wewe. Leo naomba uweke mtu kwa mapito yangu ambaye naweza agiza kwa niaba Yako. Nipe maneno, kukubali na ujasiri wa kufanyika shahidi.

*Masomo ya leo:*

Matendo ya Mitume 9:6, 17; Lakini simama sasa, uingie mjini na huko utaambiwa unachopaswa kufanya." Basi, Anania akaenda, akaingia katika hiyo nyumba. Kisha akaweka mikono yake juu ya Saulo, akasema, "Ndugu Saulo, Bwana ambaye ndiye Yesu mwenyewe aliyekutokea ulipokuwa njiani kuja hapa, amenituma ili upate kuona tena na kujazwa Roho Mtakatifu."

Matendo ya Mitume 10:5-7; Sasa, watume watu Yopa wakamwite mtu mmoja aitwaye Simoni, kwa jina lingine Petro. Yeye yumo nyumbani kwa Simoni mtengenezaji wa ngozi ambaye nyumba yake iko karibu na bahari." Huyo malaika aliyesema hayo alipokwisha kwenda zake, Kornelio aliwaita watumishi wawili wa nyumbani na mmoja wa askari zake ambaye alikuwa mcha Mungu,